GATUNDU DISTRICT
EVALUATION TEST
STD. 5 END OF TERM II 2010 KISWAHILI

Ziba mianya kwa maneno yafaayo

Polisi wanasaka genge __1__ majambazi __2__ ambao walimdunga mwanafunzi __3__ yenye sumu alipokuwa akienda shuleni wilayani Mwingi.

Polisi wanashuku ilikuwa ni njama ya kumteka nyara mwanafunzi huyo na __4__ kudai pesa za kumkomboa kutoka kwa familia __5__.

Mwanafunzi huyo wa darasa la tano katika shule ya msingi ya Kathiani alipatikana na majambazi __6__ mwendo wa saa kumi na mbili asubuhi. Watu walioshuhudia tukio hilo walipiga mayowe. __7__ ya majambazi hao kutoroka na kumwacha akiwa hoi," Mkuu __8__ polisi tawala wilayani, __9__ James Mutua alieleza. __10__ mwanafunzi huyo alipelekwa hospitali akiwa amepoteza fahamu.

1. A. cha B. la C. wa D. na
2. A. wanne B. nne C. wane D. nine
3. A. sidano B. shindano C. sindano D. chindano
4. A. kichaa B. kicha C. kisha D. kisa
5. A. wake B. yake C. lake D. lao
6. A. hawa B. wao C. hao D. wale
7. A. baadaye B. baada C. kabla D. bada
8. A. wa B. la C. cha D. mwa
9. A. bi B. bibi C. bwana D. binti
10. A. atasema B. alisema C. anasema D. amesema

Basi __11__ zamani za kale, paliondokea msichana __12__, jina __13__ Dhahabu, Alikuwa kipusa. Lo! __14__ Aliumbwa akaumbika. __15__ mwana wa pekee wa mzee Heshima na Bi Vumilia.

11. A. kule B. huku C. hapa D. hapo
12. A. mmoja B. mumoja C. moja D. mojamoja
13. A. langu B. yangu C. lake D. yake
14. A. . B. ! C. ? D. ”
15. A. anakuwa B. alikua C. anakua D. alikuwa

Kuanzia swali 16 hadi 30 jibu kulingana na maagizo

16. ***Andika sentensi ifuatayo katika wingi***
Kipepeo huyu wangu ni maridadi
A. vipepeo hawa wangu ni maridadi
B. vipepeo hivi vyangu ni maridadi
C. kipepeo hiki kyetu ni maridadi
D. vipepeo hawa wetu ni maridadi

17. ***Tumia amba ipasavyo***
Cherehani hushona vizuri ni hiki
A. ambacho B. ambalo
C. ambazo D. ambacho

18. ***Kanusha sentensi ifuatayo***
Kiti hiki kimevunjika
A. kiti hiki hakivunjiki
B. kiti hiki hakijavunjika
C. kiti hiki hakikuvunjika
D. kiti kile kimevunjika

19. ***Tegua kitendawili hiki***
A chora lakini hajui achoracho
A. mtoto B. kalamu
C. konokono D. kipofu

20. Jumla ya silabi katika mshororo wa shairi huitwa
A. mizani B. vina
C. ubeti D. kibwagizo

21. ***Tumia kiulizi PI ipasavyo***
Ni mgonjwa ____ aliyelazwa jana?
A. upi B. ipi
C. yupi D. kipi

22. Chagua msamiati wa mavazi katika makundi haya
A. suti, surupwenye, manati na zulia
B. joho, pamba, kitambaa na jezi
C. kitenge, msumeno, korosho na buli buli
D. Buibui, joho, tarbushi na kitenge

23. Ni sentensi ipi iliyoandikwa katika jinsi ya tendewa
A. babu amepigiwa simu
B. babu amepiga simu
C. babu amepigwa na simu
D. simu imepigwa na babu

24. ***Kamilisha tashbihi ifuatayo***
Eupe kama _____
A. maziwa B. meno
C. pamba D. theluji

25. ***Chagua matumizi mwafaka ya NDI kwenye mwanya***
Maji haya _____ yaliyochotwa na dada
A. ndio B. ndiyo
C. ndie D. ndizo

26. Akisami $\frac{1}{8}$ huandikwaje kwa maneno
A. thumuni B. thuluthi

C. sudusi D. tasa

27. Dadake mme wa mtu huitwa
A. dada B. mwamu
C. mpwa D. wifi

28. Sehemu ya sikio inayoning'inia na huvalishwa vipuli huitwa
A. masikio B. ndewe
C. kisogo D. kope

29. Wakati wa mafuriko huitwa msimu wa
A. kiangazi B. kipupwe
C. masika D. vuli

30. Chagua sentensi iliyotumia kiswahili sanifu
A. magari kumi na tatu yamepitia hapa
B. wasichana wasita ndio wanafagia darasa
C. viti saba vimeletwa ofisini
D. milango tano imetengenezwa upya

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu swali la 31 - 40

Pulika nikieleza, yaliyo mwangu moyoni
Nawala hayana kiza, si chochezi asilani
Yampasa kujikaza, vya muhimu fahamuni
Vyakula vya kiasili, tiba ya mengi magonjwa

Vya sukari vingi twala, hatujali madharayo
Mafuta twapenda kula, chunga aina ulayo
Hospitali twalala, ijapo dawa tunayo
Vyakula vya kiasili, tiba ya mengi magonjwa

Tupeni wenu ujuzi, mlio wataalamu
Tuifanye sote kazi, tunapopata elimu
Kuhimiza vya azizi, ni letu sote jukumu
Vyakula vya kiasili, tiba ya mengi magonjwa

Beti nne nazibwaga, haki tumeshazinduka
Matunda nafaka mboga, vya mizizi ukitaka
Na vya kemikali aga, vilivyo katika duka
Vyakula vya kiasili, tiba ya mengi magonjwa

31. Shairi la aina hii huitwa _____
A. takhmisa B. tasdisa
C. tarbia D. tathlitha

32. Shairi hili lina beti _____
A. kumi na sita B. nne
C. nane D. kumi

33. Kibwagizo cha shairi hili ni _____
A. pulika nikieleza, yaliyo mwangu moyoni
B. vya sukari vingi twala, ijapo dawa tunayo
C. beti nne nazibwaga, haki tumeshazinduka
D. vyakula vya kiasili, tiba ya mengi magonjwa

34. Shairi hili lina mistari mingapi katika kila ubeti?
A. minne B. minane
C. sita D. kumi na sita

35. Mstari wa shairi huitwa _____
A. mizani B. mshororo
C. vina D. beti

36. Kila mstari una mizani _____
A. nane B. nne
C. kumi na sita D. kumi

37. Mstari wa kwanza katika ubeti wa pili, tunaonywa juu ya madhara ya vyakula vyenye _____
A. mafuta B. tiba
C. dawa D. sukari

38. Taja vina vya ndani na nje vya ubeti wa nne
A. ga, ka B. za, ni
C. zi, mu D. la, yo

39. Katika ubeti wa nne, tunashauriwa _____
A. tusile vyakula vya mizizi
B. tule matunda nafaka na mboga
C. tule vyakula vya kemikali
D. tule vyakula vya kiasili

40. Kwa jumla, shairi hili ni juu ya _____
A Hospitali zetu nchini
B. Aina za mashairi
C. vyakula vya kiasili kama dawa
D. Dawa za kulevya

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuatayo 41 - 50

Mzazi ni mungu wa pili, naye mwalimu ambaye ni mzazi wa shuleni anaweza kusemekana kuwa mungu wa tatu. Wawili hao ndio walezi wa watoto wakiwa nyumbani na shuleni, mtawalia. Jina baba au mama ni jina la heshima linalopewa mtu yeyote mwenye jukumu la kulea na kumwelekeza mtoto na jamii kwa ujumla. Sio lazima mlezi huyo awe mzazi wa damu. Anaweza kuwa baba au mama wa kambo, shangazi, mjomba, ndugu, dada au hata binamu. Mwalimu kwa upande mwingine, ni jina la heshima linalopewa mtaalamu anayepaswa kukuza akili za wanafunzi na kuwaelekeza maishani. Wawili hao wana jukumu waliowekewa, kwanza na Mungu, na pili na jamii, kuwaelekeza wale walio chini yao kwa cheo na umri hasa watoto. Mzazi ana jukumu la kuwalea wanawe kwa kuhakikisha wamekula, wamevaaa, wana mahali pa kulala na wameenda shuleni. Mwalimu, kwa upande wake, anajukumu la kuhakikisha wanafunzi wanajifunza wasioyajua maishani mbali na kuelekeza tabia na mienendo yao wakiwa shuleni.

41. Katika taarifa hii ni nani mzazi wa tatu _____?
A. Mungu B. Mwalimu
C. Daktari D. Jaji

42 Kulingana na habari hii wazazi wa watoto nyumbani ni _____
A. mzazi, mwalimu
B. mzazi, mkulima
C. mkulima, bawabu
D. Bawabu na mwalimu

43. Neno jingine lenye maana sawa na Mungu ni ____
A. Shetani B. Ibilisi
C. Mola D. malaika

44. Kamilisha methali hii: Mama wa kambo
A. ni mzuri B. si mama
C. ni kisirani D. ni mama pia

45. Shangazi, dada, ndugu, binamu wote ni ____
A. watu B. wazee
C. wahenga D. ukoo

46. Jukumu la kukuza akili za mtoto ni la _____
A. mwalimu B. kiranja
C. mzazi D. mhazili

47. Kiongozi wa wanafunzi darasani au shuleni ni ____
A. bawaba B. mtawala
C. kiranja D. kiongozi

48. Majukumu ya mzazi yaliyotajwa katika habari ni mangapi? _____
A. matano B. manne
C. mawili D. sita

49. Kutokana na habari ulioisoma jukumu la mwanafunzi shuleni limetajwa kuwa ni _____
A. kujifunza asiyoyajua B. kupoteza wasaa
C. kutotii walimu D. kuzozana

50. Kichwa mufti kwa habari ulioisoma ni _____
A. mtoto na mwalimu B. mungu na mtoto
C. Baba na mtoto D. malezi ya watoto